

Uhuru wa Utendaji wa Mashairi ya Harusi ya Waswahili katika Miktadha ya Kiisilamu

Mwamzandi, S.Y.[1], Wafula, M.[2], Kandagor, M.[3]

IKISIRI

Makala haya yamechunguza uhuru wa utendaji wa mashairi ya harusi ya Waswahili katika miktadha ya Kiisilamu. Azma yake kuu ni kuchanganua uhuru wa mshairi katika utunzi na utendaji wa mashairi ya harusi katika jamii ya Waswahili na kutilia manani miktadha ya Kiisilamu. Kupitia mashairi teule; Wapeni Njia Warembo la Ukhty Dida kutoka Zanzibar na Nataka Kuunda la Bi.Rahma na wenziwe kutoka Kenya uhuru huu wa utendaji wa mashairi haya uliweza kubainishwa. Mwandishi aliongozwa na nadharia ya Uhistoria Mpya kuchanganua uhuru wa utendaji katika mashairi haya kwa kuwa nadharia hii inatilia mkazo umuhimu wa muktadha, historia na utamaduni wa jamii katika utunzi na uhakiki wa kazi za kifasihi. Utafiti nyanjani na mtandaoni ulitumika ili kupata data. Shairi la Wapeni njia Warembo likapatikana kupitia mtandao wa Youtube. Huku shairi la Nataka Kuunda kutoka Kenya likapatikana baada ya mtafiti kuzuru maeneo ya Malindi, Kenya akahoji pamoja na kushuhudia utendaji wa shairi hili Kupitia makala haya tuliweza kubaini kuwa miktadha ya Kiisilamu kamwe haijakuwa kuzuizi katika uwasilishaji wa mashairi ya harusi ya Waswahili. Watunzi waliweza kutumia uhuru wao sio tu kwenye utunzi wa mashairi haya, bali pia katika utendaji wake. Makala haya ni muhimu katika uwanja wa fasihi hasa ushairi kwani yanatoa mchango katika maendeleo ya ushairi na hatua zilizopigwa katika uwasilishaji wa mashairi ya Waswahili katika miktadha nyeti kama ya Kiisilamu.
Maneno muhimu: *uhuru, utendaji, utunzi, miktadha.*

1.0 Utangulizi

Katika hatua muhimu za kimaisha miongoni mwa tamaduni za Waswahili, ndoa na harusi ni mojawapo. Harusi ni moja kati ya sherehe pendwa katika jamii ya Waswahili. Ni sherehe ambayo hufanywa ili kusherehekea ndoa kati ya msichana na mvulana ambao wamefikia umri wa kuoana. Tena ni miongoni mwa sherehe kubwa ambazo hufurahiwa kwa kualika watu mbalimbali wakiwemo ndugu, jamaa na marafiki. Sengo (1992:53) akirejelea maoni ya (Mbaabu 1985) kuhusu harusi na ndoa anaeleza kuwa Uswahilini ndoa na harusi ni taasisi ya kwanza kwa uzito wa maisha ya kila siku ya mtu. Wanaendelea kusema kuwa ni desturi iliyoenea mwote Uswahilini, kwa wazazi kuwa washauri wakuu wa ndoa za watoto wao.

Licha ya kuwa ni shughuli kubwa na nzito, shughuli hii hupendelewa zaidi kuliko zingine na moja ya sababu kuu ya kufanya ipendelewe ni zile sherehe na matukio yanayohusishwa nayo. Matukio mengi kama vile singo, kunyoza, kupamba, kudondoa mchele, kufunga na kufungua begi la biharusi, hidaya, nikkah, upakaji hina na kadhalika hufanywa kwa matumbuizo mbalimbali yanayohusu uimbaji, upigaji ngoma na uchezaji. Harusi hivyo, huhusisha pakubwa utunzi na utendaji wa mashairi ya Kiswahili katika miktadha mbalimbali kutegemea mapendeleo na matakwa ya jamii au familia husika.

Tukirejelea jamii ya Waswahili kwa ujumla, utunzi wa mashairi, uimbaji na utendaji wake katika sherehe za harusi umekuwa desturi kuu ambayo haijaanza tu juzi bali imekuwa kwa kipindi kirefu. Matukio haya katika hatua mbalimbali za harusi huwa na majukumu mbalimbali kimila na desturi za Waswahili. Baadhi ya majukumu haya ni mosi, kukamilisha zile ada ndogondogo zinazofungamana na shughuli nzima ya harusi. Mfano, kuimba na kucheza (*ndundu)*wakati wa kudondoa mchele, uimbaji na uchezaji wa *sasambu* wakati wa kufungua *begi* la biharusi, uimbaji na uchezaji wa mgeni kangia wakati biharusi anaingia katika boma la mumewe n.k.
Jukumu la pili ni kuwa mashairi haya au nyimbo hizi hutumiwa kama kiashiria cha kuwa sasa ni wakati wa tukio fulani au tukio fulani linatendeka. Hivyo uimbaji na utendaji wa nyimbo au shairi fulani hutoa taarifa kwa hadhira juu ya tukio linalotendeka au linalotaka kutendeka katika kipindi kile. Wanaohusika hivyo husongea karibu na wasiotakikana kuwepo katika kipindi kile huondoka. Tatu, mashairi haya hutungwa na kutendwa kwa malengo ya kuwafunda,kuwahusia na kuwaelekeza maharusi kuhusu suala zima la ndoa (namna ya kuishi kama mume na mke). Wakati mwingine tungo hizi huwasilishwa kama zawadi kwa maharusi.

Jukumu la mwisho ni kuwa tungo hizi hutungwa, kuimbwa na kuchezwa kama burudani katika kipindi hiki cha sherehe.

Shamrashamra za harusi hata hivyo hasa utunzi na utendaji wa mashairi hutegemea muktadha husika. Kama wanavyoeleza (Mumbo na Indede, 2004) wakiwanukuu (Njogu na Chimerah, 1999) wanadai kuwa muktadha ni mazingira ya kihistoria, kijiografia, kisiasa, kiuchumi na kiutendaji yaliyozua tungo husika. Wanaendelea kwa kusema kuwa muktadha pia hurejelea yaliyomzunguka mwandishi wakati wa utungaji wake na kufichua masuala muhimu ya kazi ya fasihi katika viwango vya fani na maudhui. Fredrich (1986) kwa upande mwingine anadai kuwa muktadha ni suala linalohusu mazingira yanayomzunguka binadamu ama mwandishi wakati wa uandishi wa kazi husika. Kutokana na maelezo haya ni bayana kuwa muktadha ni kipengele muhimu katika utunzi na uwasilishaji wa kazi mbalimbali za kifasihi. Mara nyingi muktadha hutumiwa kwa ujumla kurejelea mazingira yaliyomzunguka na aliyorejelea mtunzi katika kazi yake husika.

Kadhalika, muktadha huwa kizingatio muhimu hasa katika uwasilishaji wa ujumbe, mawazo au fikra za kazi zao. Hali hii hivyo imepekelea watunzi wengi kuwa makini hasa wanapowasilisha kazi zao katika hadhira zao mbalimbali. Uwasilishaji wa kazi kulingana na muktadha huwa na lengo la kuhakikisha kuwa ujumbe umetendewa haki, umewasilishwa, umefikia na umeeleweka ipasavyo katika mazingira na hadhira iliyokusudiwa. Kupitia maelezo, muktadha unaonekana kuwa kama 'kifungo' katika utunzi na utendaji wa mashairi tunayorejelea. Hivyo basi tutachunguza namna watunzi na watendaji wa mashairi haya katika muktadha husika ambao ni wa Kiisilamu wamejinasua kutoka kwa kifungo hiki ili kufurahisha hadhira zao.

Ingawa Waswahili ni watu ambao wanaongozwa na mila zao asili na dini ya Kiisilamu, masuala mbalimbali ya kitamaduni huwatambulisha ila Uisilamu ni kitambulisho chao ambacho hakiwezi kutenganishwa nao. Harusi zao hivyo hufanywa kwa kuzingatia haya. Kuna ambao wataegemea sana kwenye Uswahili na wale ambao watazingatia dini zaidi. Kutegemea na matakwa, mapendeleo na mitazamo ya wahusika na miktadha mbalimbali, harusi inaweza kufanywa kwa *uimbaji wa Taarabu/bongo fleva au usomaji wa Kaswida*. Utunzi na utendaji wa mashairi ya harusi hutofautiana kutokana na muktahdha. Ikiwa muktadha ni wa Kiisilamu kunakuwa na - usomaji wa mashairi ambayo wengi huyarejelea kama 'kaswida' .
Na ikiwa muktadha ni wa kijamii zaidi basi uimbaji wa taarabu hupendelewa zaidi. Katika muktadha wa Kiisilamu, mashairi ya Kiswahili ya harusi hutungwa na kuwasilishwa kwa namna maalumu. Utunzi wake kwa mfano, hufanywa kwa kufuata baadhi ya sheria za msingi za utunzi wa kaswida za Kiarabu ambazo ni pamoja na;

i. Kuanza kwa jina kwa jina la Mungu.
ii. Kumsimfu mtume na maswahaba wake.
iii. Kuendeleza na kuhubiri mafundisho ya dini ya Kiisilamu.
iv. Vilevile tungo hizi kuandikwa kwa hati za Kiarabu n.k.

Utendaji wake nao hufanywa kwa mazingira ya Kiisilamu zaidi na baadhi ya mambo yanayohusishwa na utendaji wa mashairi haya katika muktadha wa Kiisilamu ni kama;

i. Usomaji ndio istilahi inayotumika zaidi kurejelea uimbaji wa mashairi katika miktadha ya Kiisilamu. Kwa sababu sio tu uimbaji bali kuna kusoma kwa *milango* (vifungu vya dua na kurani) ili kuombea maharusi baraka kwa Mungu.
ii. Mavazi yenye heshima na stara kama ilivyoelezwa katika dini ya Kiisilamu. Hivyo basi, utakuta katika harusi nyingi za miktadha ya Kiisilamu wanawake wamejistiri kwa magauni marefu na kusitiri vichwa vyao na mitandio licha ya kuwa wamejipamba kwelikweli.
iii. Kucheza ni kwa kistaarabu na wasomaji mashairi na hadhira hucheza wakiwa wamekaa huku wakiyumbayumba na kujizugazuga wakifuata midundo ya matwari/dufu na visinia.
iv. Hadhira iwe ya Waisilamu n.k.

Makala haya hivyo yamechunguza uhuru wa utendaji wa mashairi ya harusi za Waswahili katika miktadha ya Kiisilamu kwa kuyachambua mashairi mawili ya watunzi kutoka nchini Kenya na Tanzania na kudondoa baadhi ya mambo ambayo yanarejelewa kuwa *"uhuru"* katika utunzi na utendaji wa mashairi haya. Kazi nyingi za kifasihi hutungwa kwa kuzingatia miktadha anuwai ambamo zimetoka. Hii ndio sababu kubwa inayopelekea wanafasihi wengi wakiwemo Njogu na Chimerah (1999) kukubali kuwa hakuna kazi ya fasihi inayotoka katika ombwe tupu. Kila mtunzi huzingatia muktadha na kuumba au kutunga kazi zake akichochewa na mazingira mbalimbali yaliyomzunguka.

2. Mapitio ya Maandishi

Masuala mengi ambayo yamefanyiwa uchunguzi na bado yanafanyiwa uchunguzi katika ushairi wa Kiswahili ni kama fani na mtindo, maudhui, maendeleo ya ushairi na uhuru wa mshairi au uhuru katika ushairi. Uhuru huu ambao huangaziwa na watafiti mbalimbali hata hivyo unaweza kutofautiana kwa namna moja ama nyingine kutegemea mitazamo yao. Mtazamo wa kwanza ni wa wanajadi kama Robert (1958), Mnyapala (1970) na Abdalla (1973), uhuru huu uko katika mipaka ya sheria za kiarudhi unaotumika na mtunzi katika kurahisisha utiririkaji wa vina na mizani bila kuharibu maana. Mfano wa uhuru wa aina hii ni kama uvunjaji wa kanuni sarufi, uongezaji na ufupishaji wa maneno na kadhalika.

Mtazamo wa pili wa uhuru katika ushairi ni ule uliozungumziwa na wanamapinduzi kuanzia mwaka wa (1970) na wataalamu kama Kezilahabi (1974) na Mulokozi na Kahigi (1979) ambao waliipanua dhana hii kwa kusisitiza kuwa uhuru katika ushairi sio tu kufupisha maneno bali ni uhuru wa mshairi kujinasua kutoka kwenye kifungo cha arudhi. Baadhi ya mambo walioshughulikia wanamapinduzi kuhusiana na uhuru kwenye ushairi ni uhuru wa mshairi kutumia muundo wa kuendana na hisia za mshairi na uhuru katika uwasilishaji wa mawazo.

Mitazamo hii ndiyo iliyopelekea Matundura na Wenzake(2017) kutafitia suala la mgogoro wa ushairi ushairi miaka hamsini baadaye. Katika kazi yao alijaribu kuchunguza sababu zilizopelekea kuwepo kwa migogoro hii huku wakitaja siasa kama chanzo kikubwa cha mgogoro huu. Kwa upande wao, wanamapokeo au wahifadhina wanatilia mkazo uzingativu wa sheria za kiarudhi wakati wa utunzi wa mashairi ya kiswahili huku wana -sasa kama Shariff (1988) wakidai kuwa kutunga kwa kufuata taratibu za muundo wa tungo za Kiswahili kuliwanyima uhuru wa kutunga. Ingawa kuna mitazamo miwili hivi sasa utendaji wa mashairi ya Kiswahili, watafiti wachache sana wameangazia uhuru huu wa wanamapinduzi/wanausasa. Uchunguzi wa uhuru wa ushairi wa kimapokea umefany zaidi. Baadhi ya tafiti hizi ni kama ya Munyao (2016) ambaye aliangazia uhuru wa kishairi katika utunzi wa mashairi kwa kuchanganua kazi za Sikate Tamaa na Miale ya Uzalendo. Lengo lake kuu lilijikita katika kubaini mbinu mbalimbali za uhuru wa kishairi pamoja na kueleza sababu za msanii kutumia uhuru huu wa kishairi. Mwishowe Munyao (keshatajwa) aliishia kuweka bayana uhuru wa kiarudhi huku akitaja na kueleza mbinu mbalimbali kama mazida, tabdila, inkisari, utohozi, matumizi ya lahaja n.k.

Makala haya hivyo alijikita kwenye uhuru kimapinduzi na mtafiti alipania kuchunguza zaidi uhuru kwenye utunzi na utendaji wa mashairi ya harusi katika miktadha ya Kiisilamu. Hivyo basi, tumeangazia uhuru kama uholela au ukiukaji wa sifa/sheria za kimsingi katika utunzi na utendaji wa kazi fulani. Uhuru huu uliweza pia kuangaziwa kama fursa/njia ya watunzi kuwa wabunifu katika kazi zao. Katika kazi hii hivyo, uhuru katika utunzi na utendaji umejadiliwa kwa kuzichambua kazi hizi *mbili* (*Wapeni njia warembo na Nataka kuunda*) na kuchunguza iwapo;

i. Kwa namna moja kazi hizi zimekiuka baadhi ya sheria/sifa ambazo sio faradhi ila ni bayana hasa tunaporejelea utunzi na utendaji wa mashairi ya Kiswahili katika miktadha ya Kiisilamu.

ii. Watunzi wana fursa ya kuwa wabunifu na kutumia njia mbalimbali kutunga na kuwasilisha/kuzitenda kazi zao mbele ya hadhira zao katika muktadha unaorejelewa.

Ukiukaji wa kimakusudi wa sheria hizi au ukawaida wa ufanywaji mambo umesababisha wengi kuonelea kwamba Waswahili wamegawanyika katika makundi mawili; wahafidhina na huru. Ila kwa jicho la yakini utagundua kuwa hakuna kinachopunguza dini ya mtu bali huu ni uhuru tu katika kazi za sanaa. Watunzi wa kazi mbalimbali wakiongozwa na dini na muktadha wake wanautumia uhuru wao ipasavyo kuridhisha hadhira zao kwa njia zao mbalimbali. Njia hizi ndizo zitakazoangaziwa mbeleni.

2.1 Msingi wa Nadharia

Mjadala katika makala haya umeongozwa na Nadharia ya Uhistoria Mpya iliyoasisiwa na Stephen Greenblatt mnamo mwaka 1980. Kwa mujibu wa Greenblatt (1980), mahitaji ya kijamii na kisiasa huathiri kwa kiasi kikubwa mchakato wa utoaji na upokezi wa kazi za kifasihi. Nadharia hii imejikitika katika misingi ya kifikra ya Raymond Williams na Michel Foucault (1997) ambao wanasisitiza umuhimu wa muktadha wa kihistoria katika uundaji na usomaji wa matini za kifasihi.

Uhistoria Mpya umekuwa na mchango mkubwa katika kufafanua miktadha mbalimbali inayofungamana na fasihi ya kihistoria. Wamitila (2003) anabainisha kuwa, uelewa wa kazi za kifasihi unahitaji uchunguzi wa kina wa hali na athari za mabadilishano ya kitamaduni yanayochochea uzalishaji wa kazi husika. Hii inatokana na ukweli kwamba matukio ya kihalisia iwe ni ya kijamii, kisiasa, kihistoria, au kiuchumi ndiyo yanayobeba dhamana ya kuibua fasihi. Isitoshe, mazingira ya usomaji na mwelekeo wa uhakiki wa kazi yoyote ya fasihi hujengwa na kuongozwa na jamii yenyewe.

Akiunga mkono mtazamo huu, Nasimiyu (2016) anaeleza kuwa Nadharia ya Uhistoria Mpya inashughulikia umuhimu wa muktadha katika utunzi na uhakiki wa kazi za kifasihi. Aidha, nadharia hii huweka mkazo katika mbinu zinazotumiwa kuisawiri au kuijenga upya historia. Hivyo, wana-Uhistoria Mpya huchochea uchunguzi makini kuhusu jamii halisi inayozalisha fasihi katika mazingira na majira mahususi.

Misingi hii iliyobainishwa katika nadharia hii ndio iliyopelekea uteuzi wa nadharia hii kwa sababu inatoa jukwaa mwafaka la kuchambua utendaji wa kazi za kishairi katika miktadha maalumu inayoshikiliwa na jamii lengwa, ambayo katika utafiti huu, ni jamii ya Kiislamu.

3.0 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulitumia mbinu mseto katika ukusanyaji wa data yake. Data zilizotumika katika makala haya hivyo zilipatikana kutotokana na utafiti uliofanyika nyanjani na mtandaoni. Ingawa kulikuwa na mseto huu mtafiti aliteua kimakusudi kazi kutoka maeneo ya nchi mbili yaani Pwani ya Kenya na Tanzania kwa sababu yanawakilisha maeneo ambamo ni makazi makuu ya jamii ya Waswahili.

Utafiti nyanjani ulitumiwa kupata data nchini Kenya na mtafiti alizuru maeneo ya Malindi ambapo alitumia mbinu ya mahojiano na uchunguzi shirikishi kupata data yake kutoka kwa Bi. Rahma na kikundi chake. Huku akiongozwa na maswali ambayo alikuwa ameandaa kumhoji mtunzi (Bi.Rahma) kuhusu tungo yake na utendaji wa kazi zake kwa jumla, mtafiti waliweza kupata shairi la Nataka Kuunda na akaweza pia kushuhudia utendaji wake katika shughuli ya harusi na akanasa tukio hili kwa video kupitia simu. Kwa upande mwingine utafiti mtandaoni nao ulitumiwa kupata data kutoka maeneo ya Zanzibar na hapa mtafiti alitumia mbinu ya upekuzi mtandaoni Youtube kupata shairi pendwa la harusi la Ukhty Dida la *Wapeni Njia Warembo.* Kupitia upekuzi huu mtafiti aliweza pia kusikiliza na kuona jinsi shairi hili lilivyoimbwa na kuchezwa katika shughuli ya harusi. Data hizi (mashairi pamoja na video) ziliandikwa na kunaswa/kupakuliwa na baadae mtafiti akazitumia kuchanganua uhuru wa utunzi na utendaji wa mashairi haya katika miktadha ya Kiislamu.

4.0 Uchanganuzi wa Data

Mjadala kuhusu uhuru wa mshairi ni mpana kama ilivyo dhana yenyewe ya ushairi. Watafiti wengi hata hivyo wameuchambua uhuru wa mshairi kwa kuangazia vipengele mbalimbali kama vya kimaandishi, kimaana, kimtindo, kisajili n.k. Katika makala haya, mtafiti aliuchanganua uhuru wa utendaji wa mashairi ya Waswahili kwa njia mbili; uhuru katika utunzi na uhuru katika utendaji akiongozwa na nadharia ya Uhistoria mpya kama ifuatavyo.

4.1 Uhuru wa Utendaji wa Mashairi ya Harusi ya Waswahili katika Miktada ya Kiisilamu

Uhuru wa mshairi ulioangaziwa katika utunzi ni wa kisajili zaidi. Hii ni kwa sababu mtafiti aliangazia zaidi namna watunzi walivyoitumia lugha kutunga mashairi kulingana na muktadha husika ambao ni wa Kiisilamu. Uhuru huu ulichanganuliwa kwa kuchanganua matini teule na kudondoa uholela uliotumika na watunzi wote katika utunzi wao. Kwa upande mwingine, utendaji umechambuliwa kwa kuchunguza uimbaji wa mashairi haya ya harusi ulioambatana au kufungamana na vitendo/matendo. Kanda za video ambazo mtafiti alinasa akiwa nyanjani na ambayo alipakua kwenye mtandao wa Youtube zilichanganuliwa. Yaliyochunguzwa katika utendaji kwa jumla ni namna mashairi haya yalivyoimbwa, yalivyochezwa na matendo mbalimbali ya waimbaji na hadhira husika wakati wa uwasilishaji. Katika makala haya hivyo, uhuru katika utendaji wa mashairi ya harusi katika muktadha wa Kiisilamu umedhihirika kupitia namna zifuatazo;

4.1.1 Ujanibishaji wa Tungo localization/kuswahilisha)

Ujanibishaji (localisation) au kile kinachojulikana kama Uswahilishaji katika taaluma ya fasihi ni mbinu ya kimtindo ambapo mtunzi hukiuka matumizi ya lugha asilia ya muktadha rejelewa. Mtindo huu wa utunzi hutokea pale ambapo watunzi hukiuka kutumia lugha inayoendana na muktadha rejelewa na badala yake kutumia lugha inayofahamika zaidi na hadhira. Kawaida mashairi katika muktadha wa Kiisilamu hutumia lugha ya Kiarabu katika utungaji na uwasilishaji wake kwa sababu hii ndiyo lugha inayohusishwa na Uisilamu. Mazrui (2007) anasema, katika muktadha wa Kiisilamu, Kiarabu ndicho huchukuliwa kama lugha ya msingi ya kisharia na kiibada (lingua franca ya kidini), hivyo kutarajiwa kutawala katika utunzi na uwasilishaji wa mashairi ya kidini. Ingawaje haya ndiyo matarajio ya kila utunzi wa mashairi katika miktadha hii, ziko baadhi ya tungo ambazo hutumia mchanganyiko/mseto wa lugha ya Kiarabu na lugha ya jamii husika katika utunzi wake. Hata hivyo kuna watunzi ambao hukiuka kabisa kuitumia lugha ya Kiarabu na kutumia lugha ya jamii pekeake.

Mashairi ya Kiswahili ya harusi katika muktadha wa Kiisilamu kwa mfano, idadi kubwa ya mashairi haya huwasilishwa katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo kuna baadhi ya watunzi au tungo ambazo huchanganya lugha hizi za Kiswahili na Kiarabu. Kiarabu hivyo kinaweza kutumika ila kwa uchache sana kikilinganishwa na lugha ya Kiswahili. Watunzi wa kazi ambazo zinarejelewa katika makala hii walikiuka kutumia lugha ya Kiarabu katika utunzi wa tungo zao na badala yake kutumia lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo inayotumiwa na kundi jamii/hadhira husika. Uhuru huu hutumika ili kuziba mwanya wa kimawasiliano kati ya nukuu za kidini na uelewa wa jamii. Kadhalika, uhuru huu hutumika ili kufanikisha dhana ya *Udaawa* (ulinganiaji) ambapo shairi linakuwa kama chombo cha mafunzo ya kiroho yanayoeleweka kwa urahisi na Mswahili wa kawaida bila kuhitaji mkalimani (Topan,2006).

Muktadha wa Kiisilamu hivyo, haujawafunga watunzi katika kutumia lugha ya Kiarabu, kwa namna yao wameweza kutunga tungo kwa lugha zao asili na kufanikiwa kutumbuiza na kulingania hadhira yao ambayo dini yao ni Uisilamu. Ukhty Dida kwa mfano, aliweza kutumia lugha ya Kiswahili kumpa mawaidha biharusi ya namna ya kuishi na kumtunza mume wake na kumfanya atulie kwake tu. Ukhty Dida ametumia lahaja ya Kiunguja ili kuufanya utungo wake upate uasilia wa Mswahili licha ya kuwa muktadha ni wa Kiisilamu.

Wapeni njia warembo,
Wapeni njia.
Waje mbele tuwaone,
Wapeni njia.

Bi. Rahma kwa upande mwingine ametumia Kiswahili cha lahaja ya Kibajuni na Kiswahili sanifu kwa pamoja katika utunzi wa shairi lake la *Nataka Kuunda*. Beti za awali kwa mfano, zimetumia Kiswahili sanifu huku beti za mwisho zikiwa katika lahaja ya Kibajuni.

Mfano 1: ubeti kwa lugha ya Kiswahili

Tupige vigelegele, Harusi kuishashia,
Iwe na baraka tele, Daima kufurahia.

Mfano 2: ubeti kwa lahaja ya Kibajuni

Wake hoya, hoya,
Eeee hoyaeee,
Naulie mshindo mmoya mmoya.

4.1.2 Matumizi ya Litifati

Upachikaji wa istilahi na vifungu vya maneno ya kidini umetumiwa kama mbinu ya kuoanisha tungo na muktadha wa utendaji wa Kiisilamu. Ingawa lugha kuu iliyotumika katika utunzi ni Kiswahili, watunzi wametumia ubunifu wao kwa kutupia na kuingiza maneno na vifungu (kama dua, kumtaja Mungu, hadithi na Kurani) vinavyoashiria na kurejelea Uisilamu kwenye baadhi ya beti kama njia ya kusilimisha na kuhalalisha tungo zao na kuzifanya zikubalike kimuktadha na mbele ya hadhira lengwa. Miktadha ya Kiisilamu kawaida huruhusu tungo ambazo zinakubalika Kiisilamu. Tungo ambazo ni za '*heshima*' kulingana na dini na ambazo zinarejelea mafundisho ya dini. Ingawaje hii ndio hali halisi, baadhi ya watu miongoni mwa hadhira huwa hawapendezwi na mashairi/tungo ambazo zimeegemea zaidi kwenye masuala ya kidunia kuliko ya kiroho. Watunzi hivyo, hutumia njia hii ya upachikaji na kutupia maneno au vifungu vya maneno ya kidini na dua kwa lengo la kuzifanya tungo hizi kuwa na mtazamo wa Kiisilamu zaidi na za kukubalika na kufurahiwa na wengi miongoni mwa hadhira.

Ingawa hali hii tunairejelea kama uhuru katika utunzi wa mashairi haya, uhuru huu umechangiwa pakubwa na shinikizo la kijamii ambapo sehemu ya hadhira huelekea kupuuza tungo zinazoonekana kuegemea zaidi kwenye masuala ya kidunia *(secular)* kuliko ya kiroho. Hivyo, mshairi hutumia uhuru wake kupachika maneno yenye uzito wa kiimani kama nyenzo ya kisaikolojia ya kuivuta hadhira na kuhakikisha kazi yake inakubalika kama sehemu ya mafundisho ya dini badala ya burudani tupu. Kwa kufanya hivi, mshairi anatekeleza dhana ya *'Ushairi wa Kiislamu (Islamic Poetics)'* ambapo uzuri wa sanaa hauwezi kutenganishwa na maadili ya kiimani (Knappert, 1971).

Mfano: ubeti wa 1 na wa 3 wa shairi la Rahma

1.Furaha imetwelea , Sote tulohudhuria,
Magoma yetu haya, Harusi kuitezea,
Kwa baraka za Nabiya, Ndoa yao kutimia.

3. Twawapa yetu pongezi, Yazidi yenu mapenzi,
Na kilo chema kizazi, Ilahi atakienzi,
Kwa nguvuze mwenyezi, Na baraka za kipenzi.

Katika shairi la Bi. Rahma 'Nataka kuunda' mishororo miwili ya mwisho katika beti tatu za mwanzo imemalizia kwa kumtaja Mungu na Mtume wake na vilevile kuomba dua kwa Mungu na Mtume ili ndoa ipate kutimia, kudumu na pia iwe yenye baraka tele. Licha ya kuwa mishororo ya awali hasa katika ubeti wa kwanza inazungumzia wahusika kuwa tayari na ngoma kuicheza harusi, mishororo inayoyofuata inalifinika hili kwa kuziomba baraka za mtume kukamilisha harusi.

4.1.3 Kuungaunga kwa Utungo

Hii ni njia ambayo kwamba watunzi hawa wawili wametumia katika utunzi wa mashairi yao. Mbinu hii imedhihirika kama uhuru katika utunzi kwa sababu, watunzi hawa hawajavungwa na mipaka ya umiliki wa kazi asili bali walilenga kukidhi mahitaji ya kijamii na kiibada ya hadhira zao. Matumizi ya matini nyingine ndani ya tungo mpya husaidia katika kuijengea kazi husika mashiko na kukubalika. Kwa kuwa sherehe zenyewe ni harusi, basi jukumu lao la kuifurahisha hadhira limewapelekea kuzibuni tungo zao zikawa zenye kuimbika, kuchezeka na kuchangamsha hadhira. Pia hutumiwa kuimarisha maudhui, kuchochea ushiriki na kuboresha midundo. Watunzi wa kazi tunazorejelea, ili kukidhi haja hii ya hadhira, wametumia mbinu ya kuungaunga tungo ambapo wengi hujumuisha vipande vya mashairi ambavyo sio kazi yao asili katika kazi zao na mara nyingi huwa vipande vya nyimbo/mashairi ambayo ni pendwa sana katika jamii husika.

Ikumbukwe kwamba, kuungaunga huku sio upungufu wa ubunifu, bali ni ufundi wa makusudi wa kuunganisha matini asili na matini mpya ili kuunda utungo wenye mwangwi wa kitamaduni na kidini huku ukidumisha msisimko wa sherehe. Katika kazi tunazozirejelea, Bi. Rahma na Ukhty Dida wanaanza kwa kutoa ujumbe wa mawaidha kwa biharusi kwanza kisha baadaye wakamalizia kwa vipande ambavyo vinaonyesha kuhusishwa kwa watu wengine kama mamake biharusi, mashangazi, madada na waalikwa wote kwa jumla. Mashairi yao yalitanguliza kwanza vipande vya beti za kutoa mafunzo ya ndoa kwa biharusi ambapo kila ubeti ulifuatiliwa na kiitikio. Nafasi ya kuungaunga kwa tungo ilitokea baada ya beti za mwisho na viitikio vya mashairi haya.

Mfano wa kwanza katika shairi la *Wapeni njia Warembo; Kuna maneno laini, Yatoa nyoka pangoni, Kwa mapenzi ni fasheni, Mume atabaki ndani, Ukijifanya muhuni, Ataka toroka ndani,*
Kuna wanomtamani, Ni watoto wa mjini, Itabaki laitini, Iiiiiii sisi tushamnyakua.
Tunaye mama harusi, Tunaye wetu wenyewe. Hata mkisema,
Mama harusi tunaye, wetu wenyewe. Hata mkinuna,
Mama harusi tunaye wetu wenywe.

Mfano wa pili katika shairi la Nataka Kuunda;
Twawapa yetu pongezi,
Yazidi yenu mapenzi, Na kilo chema kizazi, Ilahi atakienzi,
Kwa nguvuze mwenyezi, Na baraka za kipenzi.

Tupige vigelegele
Harusi kuishashia, Iwe na baraka tele, Daima kuifurahia

Wake hoya hoya, Eeeeh hoya eeeeh,
Leo naulie mshindo mmoya mmoya.

Kama ilivyodhihirika katika mifano hii miwili, baada ya beti za mwisho za mashairi haya, watunzi na baada ya ‘korasi/kiitikio’ watunzi wanaunga tungo zao kwa vipande vya beti ambazo huwa ‘kilele’ cha tungo na ambazo huongezwa tu kwa ajili ya kuichangamsha hadhira. Mara nyingi hazina mafunzo yoyote kwa biharusi ila huwa na lengo la kujumuisha hadhira iliyohudhuria harusini na kuwapa nafasi ya kujipumbaza, kujiliwaza,kuringa na kujishaua.

Kuungaunga kwa tungo kumefanya mada pia zikabadilika badilika. Mada ziligeuka kutoka kuwa nzito (kuhusu ndoa) mpaka kwa mada za kuhusisha hadhira kujiachia na kufarahia. Hii inatuonyesha kuwa watunzi hawajazingatia tu mhusika mkuu ambaye ni biharusi bali na wengine pia ambao huenda ikawa ndugu, jamaa au marafiki waalikwa. Kubadilishwa kwa mada na kuungwa ungwa kwa tungo ni njia vilevile ya kukidhi mahitaji ya kimuktadha kwa sababu kunaonyesha namna watunzi wanavyobadilisha kazi zao kutoka uswahilini hadi kwenye dini na kutoka kwenye dini kwenda uswahilini.

4.1.4 Utiaji Sauti

Utiaji sauti ni hatua muhimu hasa kwenye uimbaji wa mashairi ya Kiswahili hasa ya harusi. Mashairi katika harusi huimbwa kwa sauti nzuri na zenye mahadhi. Ingawaje hii ndiyo hali ilivyo, sauti ya mwanamke katika dini ya Kiisilamu husemekana kuwa *‘awra’* kwa maana ya uchi na haifai kupazwa ikasikika na wanaume ila kwa mumewe tu. Ingawa kuna unyeti wa kidini kuhusu sauti ya mwanamke, watunzi wa mashairi ya harusi katika muktadha wa Kiisilamu wamefanikiwa kuoanisha mahitaji ya kidini na hitaji la kibinadamu la kujieleza kisanaa. Hivyo, matumbuizo mengi ya harusi au utendaji wa mashairi katika harusi huhusisha uimbaji ambapo wanawake huwa huru kuimba na kufurahia harusi. Watunzi wetu tunaporejelea katika kazi hii wametumia uhuru huu kupitia njia zinazofuata;

Kwanza, walizitia tungo zao sauti zikawa ni zenye kuimbika. Na sio tu kuimbika hivi hivi, uimbaji huu ulitoka kutoka moyoni na madaha. Moja kati ya njia ambayo ilitumika ni kuongeza na kurefusha irabu hasa mwishoni mwa mishororo au ubeti. Mfano shairi la *Wapeni Njia Warembo,* mishororo miwili ya mwisho katika beti za 1,2 na 3 mtawalia.

Kamtunze mume wako,

Ooooh oooh,
Wala usiwe na wivu.
Kuna watu wamwinda,
Aaaah aaah,
Mara watamnyakua.
Utabaki laitani,
Iiiii iiiii,
Sisi tushamnyakua.

Katika shairi la Bi.Rahma vilevile njia hii ilitumika mfano katika ubeti wa 8;

Nataka kuunda ***eeeh***
Kuunda ***eeeh***
Na sina mbao ***eeeh***

Mbinu hii ya ubunaji mara nyingi hutumika katika mashairi na ngojera za taarabu ila katika kazi hii watunzi wameweza kuitumia vilevile kama njia ya kupamba tungo zaidi na kuzidisha ladha ya mashairi wakati wa uimbaji. Kadhalika, watunzi waliweza kuambatisha sauti za uimbaji na zile za ala mbalimbali. Ala za mziki kama vile madufu na vifaa vingine kama spika,piano, visinia na miko zilitumika. Miktadha ya Kiisilamu hata hivyo hairuhusu matumizi ya baadhi ya ala za mziki wakati wa uimbaji. Kitendo cha kutumia ala za miziki hasa za kisasa kama piano na gitaa katika uimbaji wa mashairi/nyimbo huwa *haramu.* Kwa baadhi ya madhehebu ya Waisilamu sio tu kutumia ala tu bali kuimba kwenyewe pia ni haramu. Watunzi wetu hivyo wamefanikiwa kukiuka na kubuni sheria na mitindo mipya kwa lengo la kukidhi mahitaji ya burudani katika shughuli za harusi licha ya kuwa miktadha inayorejelewa ni ya Kiisilamu.

4.1.5 Kurefusha kwa Kurudiarudia Beti za Mwisho

Mbinu hii imetumiwa na watunzi wote wawili hasa wakati wa uimbaji wa mashairi yao. Watunzi hawa walizirefusha na kuzirudia beti hasa za mwisho zaidi ya mara moja. Kilichobainika ni kuwa beti zilizorejelewa na kurudiwa ni zile 'korasi/viitikio' vya mashairi haya. Wanaongoza uimbaji wa mashairi haya (Ukhty Dida na Bi. Rahma) waliongoza kisha waitikaji ambao huimba korasi/viitikio tu wakafuatiliza. Kadhalika, zile sehemu ambazo hadhira zilionekana kufurahia zaidi wakati wa uimbaji hususani zile zilizoungwaungwa zilirudiwa pia na kuimbwa kwa urefu. Hali hii imedhihirika vilevile katika mashairi yetu na watunzi walirudia beti zilizopo hapo chini zaidi ya mara tatu huku upigaji wa madufu na ala mbalimbali ukiwa ukianza polepole kisha kubadilika na kuwa wa kasi mno kuambatana na uimbaji.

Wapeni njia Warembo:
Tunaye mama harusi, Tunaye wetu wenyewe.
Hata mkisema,
Mama harusi tunaye, wetu wenyewe. Hata mkinuna,
Mama harusi tunaye wetu wenywe.

Mfano, Nataka kuunda:
Tupige vigelegele Harusi kuishashia, Iwe na baraka tele, Daima kuifurahi.

Uhuru huu ambao watunzi hawa wawili wametumia kipindi cha utendaji (uimbaji) umetumimika kuashiria kuwa muimbaji amefika kilele cha matumbuizo yake na anakaribia kumaliza. Hadhira huonyesha kupandwa na mori na hili huwa kusudio kubwa la waimbaji. Marudio haya na urefushaji huu husababisha mihemko na watu huwa huru hata katika kucheza kwao wakaweza kucheza na kuitikia kwa namna wanavyojisikia katika wakati ule.

4.1.6 Uchezaji

Nafasi ya msanii katika utendaji ni kubwa ikilinganishwa na ile ya hadhira kwani yeye ndiye atakayeifanya harusi ifane au ipumbae. Licha ya wengi wao kubanwa na miktadha mbalimbali ya utendaji, wengi huwa na jukumu la kuhakikisha kuwa hadhira imefurahi, imeshiriki na walilolitarajia limefanikishwa na kuwasilishwa ifaavyo. Hali hii tunaiona kupitia namna watunzi waupa uchezaji nafasi katika kazi zao hasa kipindi cha uwasilishaji kwa hadhira. Kawaida uimbaji hasa wa nyimbo na mashairi katika muktadha wowote ule huhusishwa na uchezaji. Uchezaji unaweza kufuata hatua mahususi au ukawa wa kiholela tu. Midundo kutoka kwenye ala mbalimbali za mziki huwa kama kichocheo au msukumo wa watu kucheza. Bila kujijua hadhira huonekana ikishiriki kucheza na huwa kama namna ya wao kuitikia, kukubali na kuguswa na kile kinachoimbwa. Wakati mwingine utakuta hadhira ikiiga hatua za uchezaji kutoka kwa watumbuiza.

Katika miktadha ya Kiisilamu, uchezaji huruhusiwa tu ila kwa namna fulani. Uchezaji wa namna ya kuyumbayumba huruhusiwa zaidi na huonekana kama uchezaji wa kistaarabu hasa dini inapohusika. Mara nyingi hakuna kurukaruka wala kuchezesha viungo vya mwili. Watu hucheza wakiwa wamekaa chini au kusimama na kuonekana kuyumba au kusongea kwenda kulia na kushoto. Vilevile katika mkusanyiko wa wake na wanaume, wanawake hawaruhusiki kamwe kucheza. Katika miktadha mingine uchezaji wenyewe huruhusika tu katika mkusanyiko wa wanawake pekee.

Katika utendaji wa mashairi teule, uchezaji wa mashairi haya katika miktadha ya Kiisilamu uliambatana na mambo mbalimbali ambayo yalichochewa na waimbaji wakati wa uimbaji wao. Baadhi ya mambo haya ni kama vile, kuchezesha na kuzungusha mikono/vidole na upigaji makofi. Tukirejelea uchezaji katika miktadha ya Kiisilamu, kucheza kwa kuzungusha mikono, vidole na kupia makofi sio kawaida ila ni mambo ya kawaida hasa wakati wa uchezaji wa nyimbo/mashairi ya taarab. Watunzi wameashiria uchezaji wa namna hii kwa hadhira zao kama njia ya kuwakumbusha kufurahi na kuonyesha maringo (mashauzi/mashauo). Mikono hurushwa juu mfano wa kupepea hivi. Msomaji Ukhty Dida ameonekana kutumia uchezaji huu na hadhira yake ikiigiza. Hadhira inaonekana kujiunga naye kupepea mikono huku wakicheza taratibu na kuitikia wimbo. Kwa walioguswa zaidi na usomaji wa mashairi haya, utaona wanazungusha kidole cha shahada huku wameinamisha nyuso zao na wengine kuzungusha pesa kuelekea kwa wasomaji mashairi na kuwatuza.

4.1.7 Uigizaji

Mbinu hii ilitumika na watunzi wakati wa uwasilishaji wa kazi zao. Uigizaji huu ulikuwa wa matendo mbalimbali ambayo yaliendana na kile kiliichoimbwa mfano, kupiga vigelegele, kucheza, kunyakua, kupandwa na presha, kutikisa mabega na kadhalika. Mfano, katika kazi ya Ukhty Dida, ukumbi ulifunguliwa na waimbaji kwa kuigiza kwa namna mbalimbali na kwa matendo ambayo yaliendana na yale waliyoimba. Ishara ya kuita hadhira mbele na kuipa njia (warembo) kwa kutumia mkono iliwahamasisha wengi kuinuka na kwenda mbele kucheza pamoja nao. Kwa kutizama video yake utakuta akianza kuimba hadhira
imekaa kwanza kisha baadaye wengi miongoni mwa hadhira wanajiunga na waimbaji kucheza na wengine wakiiga kila wanachokifanya.

Vigelegele pia vilishuhudiwa kwa wingi katika utendaji wa mashairi yote. Vigelegele ndio kelele za harusini. Ni sauti zinazotolewa kinywani kwa kuchezesha ulimi na kuziba mdomo kwa mkono hasa na wanawake. Sauti hizi hutumiwa kama ishara ya furaha au shangwe. Miktadha mingi ya harusi hutumia sauti hizi kuashiria kufanikishwa kwa jambo, furaha au kama kiitikio tu. Katika tungo zetu, hasa kwenye ushairi wa Bi. Rahma, vigelegele vimetumika sana kwenye utendaji na pia kimaandishi. Kipande cha korasi '*vigelegele kwa sana*' kilipoimbwa, baadhi ya waimbaji walipiga vigelegele na hili lilichochea baadhi ya watu kwenye upande wa hadhira kuiga pia.

Kupiga makofi katika arusi za miktadha ya Kiisilamu ni jambo ambalo lilidhihirika. Kikundi kilichoongozwa na Bi. Rahma katika usomaji wa shairi lake, licha ya kutumia madufu, visinia na miiko, walitumia makofi vilevile ambayo yalipigwa yakiambatana na midundo ya ala nyingine na uimbaji wenyewe. Hali hii ilitumiwa kama njia ya kushangilia na kuwapa motisha waimbaji. Ilibainika kuwa wakati makofi yalipigwa, waimbaji walizidisha madoido kwenye uimbaji wao. Hadhira vilevile ilionekana izaji wao walifanya. Hadhira ilipiga makofi kwa muongozo wa waimbaji na wasindikizaji wao.

4.1.8 Hadhira

Hadhira katika miktadha ya Kiisilamu huwa na sharti moja kuu ambalo ni kutokuwepo na mchanganyiko wa wanawake na wanaume. Na ikiwa utakuwepo basi wanawake wakae kando na hadhira ile ya wanaume. Hivyo basi, utakuta wakati wa uwasilishaji wa mashairi katika miktadha ya Kiisilamu, watendaji/wawasilishaji wa kike mara nyingi huwa na hadhira ya kike pekeake na wa kiume vilevile na mara chache mjumuiko wa wote wakitenganishwa na nafasi baina ya wanawake na wanaume.

Hadhira katika shairi la *Nataka Kuunda* ilifanikiwa katika utekelezaji wa sharti hili la hadhira kwa msingi ya dini kwa sababu watendaji waliwasilisha kazi yao mbele ya hadhira ya kike tu. Kwa upande mwingine katika moja ya video za uwasilishaji wa shairi la *Wapeni Njia Warembo* hadhira inaoneka kuwa ya mchanganyiko wa wake na wanaume. Mipaka hii ya hadhira kulingana na muktadha wa Kiisilamu imekiukwa na watendaji na sababu huenda ikawa miongoni mwa watendaji ni wanaume pia ambao walikuwa wakicheza ala mbalimbali. Kilichobainika hata hivyo ni kuwa hadhira na watendaji wote kwa jumla waliweza kujisitiri vizuri na hata watendaji kuonekana kuweka mipaka kwenye ukaaji stejini. Wanaume walikaa mbali na wanawake.

5.0 Hitimisho

Makala haya yalilenga kutathmini uhuru wa utendaji wa mashairi ya harusi ya Waswahili katika miktadha ya Kiiisilamu. Kutokana na tathmini yetu, ilibainika kuwa ingawa miktadha ni muhimu sana katika utunzi na utendaji wa mashairi haya, watunzi wana uhuru wa kubuni upya au kufanya uholela wa namna mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya hadhira zao. Kupitia makala haya tumeona jinsi watunzi wa mashairi ya harusi katika miktadha ya Kiisilamu walivyoweza kutumia uhuru katika kuyatunga na kuyawasilisha mashairi yao kwa njia mbalimbali. Kwingine iliwalazimu kukiuka na kufanya mambo kiholela na vilevile kuwa wabunifu ili kutekeleza jukumu lao kama watoa burudani katika shughuli husika. Mbinu zilizotumiwa zilionyesha namna hadhira walivyofurahia na wakaweza pia kujuimika na watendaji kwa kucheza vile walivyoweza na kujisikia. Hali hii ilizipa hadhira uhuru na nafasi ya kushiriki bila kubanwa na muktadha wa Kiisilamu. Uhuru huu vilevile uliweza kuipa hadhira nafasi ya kuingilina na tungo hizi kwa kiwango fulani hivyo kuwapa watendaji fikra ya kuwa wamefaulu katika kuuwasilisha ujumbe ilivyostahiki.

Acknowledgement

This article is the outcome of research conducted within the Africa Multiple Cluster of Excellence at the University of Bayreuth, funded by the Deutsche Forschungsgemeinschaft (DFG, German Research Foundation) under Germany's Excellence Strategy (EXC 2052/1 – 390713894).

MAREJELEO

Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki*. Oxford University Press.

Abdallah, R. O. (2024). *Nataka Kuunda.* Shairi Halijachapishwa.

Aqaz Star Maulid (2021). *Ukhty Dida Avami wa na warembo ndani ya Holi kwa Qaswida Pambe ya Kharusi.* Available at https://youtu.be/2aoaKHCTICc?si=8kHB602Vg Tj3og GD. Imepakuliwa 31/05/2025 saa 10:16.

Foucault, M. (1997). *The Order of Things*.london: Routeledge and Kegan Limited.

Friedrich, P. (1986). *The Princes of Naranja: An Essay in Anthrohistorical Method.* Austin: University of Texas Press.

Greenblatt, S. (1980). *Renaissance Self Fashioning*. Chicago: University of Chicago Press.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi.* Heinemann Educational Books. Knappert, J. (1971). Swahili Islamic Poetry. Brill.

Matundura, E na Wenzake (2017). *Mgogoro wa Ushairi wa Kiswahili Miaka Hamsini Baadaye.* Jarida la Mwanga wa Lugha.

Mazrui, A.M (2007). *Swahili Ethno-psychology and Cultural Appropriation.* Africa World Press.

Mbaabu, I. (1985). *Utamaduni wa Waswahili.* Kenya Publishing & Book Marketing Co. Ltd, Nairobi.

Mnyapala, M. E (1970). *Nguzo yaU Ushairi Kiswahili.* East African Literature Bureau.

Mulokozi, M. Na Kahigi (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu.* Tanzania Publishing House.

Mumbo, C.K., & Indede, F.N (2004). *Johari ya Kiswahili: Kidato cha Tatu.* Nairobi: Acme Press Ltd.

Munyao, M.K. (2016). *Uhuru wa Kishairi katika Utunzi wa Mashairi: Uchanganuzi wa Sikate Tamaa na Miale ya Uzalendo.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Nasimiyu, M.C. (2016). *Athari ya Mazingira ya Kihistoria na Kijamii katika Uwasilishaji wa Maudhui ya Dhifa* (E.Kezilahabi). Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi.

Robert, s. (1958). *Pambo la Lugha.* Oxford University Press.

Sengo T. S.Y (1992). *Utamaduni wa Kiswahili: Wilaya ya Kusini Unguja.* Katika Nordic Journal of African Studies 1 (1), 53-79.

Shariff, N.I(1988). *Tungo Zetu.*New Jersey: The Red Sea Press Inc.

Topan, F. (2006). *Why Does a Swahili Writer Write? Euphoria, Pain and Swahiliness.* Research in Literature.

Wamitila, K.W (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Focus Publication Ltd.

Zanzibar One Qaswda (2022). Ukhty Dida - *Wapeni njia warembo (Official video).* Available at https://youtu.be/JUS8wGSdY3w?si=jt6Hipz9iC53Bcks. Imepakuliwa 31/05/2025 saa 10:16.

-